# Ile Siri Ya Ubatizo Wa Roho Mtakatifu

*1Korintho 12:13*

*"Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja"*

Ni nini ubatizo wa Roho Mtakatifu? Ni Roho anapokubatiza wewe ndani ya mwili wa Kristo (1korintho 12:13). Ni kule kuzaliwa kwa pili. Ni yule Roho wa Mungu anapokuja ndani na kukujaza wewe baada ya kutubu kwako. (Ulipolisikia Neno lake) na ukabatizwa ndani ya maji kama jibu la dhamiri safi mbele za Mungu. (Matendo 2:37-41). [1]

Na sasa umali yake. Oh, kwa sababu yupo, tunazo haki zote kwa vyote Ambavyo amevinunua kwa ajili yetu. Kila Ahadi katika Biblia ni yako. Ni ya kwako. Kama ile Ishara iko juu yako na Mungu amekutia muhuri wewe. Sasa tunataka kujichunguza wenyewe kwa muda kidogo. Wakati Mungu amekupa wewe ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, hapo sasa uhai wa Yesu Kristo uko ndani yako. Sasa, hiyo ni kweli na kila mtheolojia inabidi akubali hilo. Huko ni kuzaliwa kwa pili (Yohana 3:1-8). Umezaliwa upya, na Roho Mtakatifu. Na kwa sababu Mungu amefanya hili, na unajua kwamba wewe sio mzuri kwa nafsi yako mwenyewe, na umekubali kile ambacho Mungu amefanya, halafu anakutia Muhuri wewe katika Ufalme wake, kwa Roho Mtakatifu. Na kila kitu ambacho Yesu amenunua na kukuahidi wewe, katika Biblia ni chako. Ni mali yako kwa sababu imekwisha kulipiwa. Amen. Uzima ni wangu; Amelipia huo. Uzima ni wako; amelipia huo.
(1Korintho 3:21-23). Uponyaji ni wangu; Amelipia huo. Uponyaji ni wako Amelipia huo. Uhuru ni wangu; Amelipia huo. Mbingu ni zangu Amelipia hizo. Amelipa gharama. Kila kitu alicho nunua ni chake mtu yule aliye na ile Ishara. Ameni. "Kitambulisho changu Ishara yangu", juu ya magari mitaani, katika siku ya hukumu, na nitapita juu yako (Kutoka 12:13). Amen. Kuishikilia hiyo ndani! Kushikilia ungamo lako katika Neno, kwa Yesu Kristo alikufa kwa ajili yako. Na anapofanya hivyo. Anajionyesha mwenyewe kupitia wewe. Amen. Ndiyo unapoitambua ile Ishara, Uhai ambao umechukuliwa kwa ajili ya Damu inene! [2]

sasa natakakujiweka wazi mimi mwenyewe juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini kutokana na Neno la Mungu. Siyo kutokana na mimi, na siyo kutokana na wewe, Ni kutokana na "Hii asema Bwana" au sivyo tunaongozwa kimakosa. Amen.

Kwa kuanzia na wewe utaona kuwa katika mikutano yangu ni napomaliza kuhubiri katika huduma ya kiinjilisti; au kufundisha ujumbe fulani ninatupa wavu na kukaribisha uwajibikaji kutoka kwa watu. Ninawaomba waje mbele na wapokee Roho Mtakatifu. Marafiki/ndugu zangu wapentekoste, wanaponisikia nikisema hivyo wanaamini kuwa ninawaita watu waje mbele wabatizwe na Roho Mtakatifu kwa sababu tayari wamezaliwa mara ya pili. Kwa hiyo ninapowaita wale waliojazwa na Roho Mtakatifu kuja na kushughulika na wale walioitikia mwito wa kupokea Roho, hawa watu huja mbele na kushuhulika na watu kwa namna ya kuwatia moyo kujisalimisha kwa Mungu na kuamini kunena kwa lugha. Hii imesababisha kuchanganyikiwa kukubwa na ninataka kuwaambia hasa kile ninachomaanisha. Na maanisha kuwa mwenye dhambi aje mbele na aweze kuzaliwa mara ya pili, ambako ni kule kubatizwa katika mwili wa Kristo, na Roho Mtakatifu. Ambacho ndicho kilichotendeka siku ya Pentekoste wakati kanisa lilipoanzishwa. Kwa maneno mengine, ni kuzaliwa na Roho ni kubatizwa kweli na Roho Mtakatifu. Ni kitu kimoja hicho hicho .[3]

Sasa tunaingiaje basi katika huu mwili? Wakorintho wa kwanza 12, "kwa Rohommoja sisi sote tumebatizwa kwa katika huu mwili; kwa ubatizo mmoja wa Roho Mtakatifu". Kwamba, kama unataka kuandika hilo ni wakorintho wa kwanza 12:13. "Na kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa". Na Roho ni uzima/uhai wa Kristo, hiyo ni sawa? Uhai wa Kristo! Na uhai wa mbegu yoyote……. Ambao. Alikuwa ni mbegu Neno, akileta uhai kwenye mbegu (Matendo 10:44-48). Unalipata hilo? Kama huo uhai uko katika mbegu, na huu ubatizo wa Roho Mtakatifu unakuja juu ya hiyo, inalazima ya kuleta ule uhai wa mbegu. [4]

Sasa kule kubadilishwa ni nini? Tunakupataje? Ni kitu gani kinaleta kubadilishwa? (Warumi 12:1-2). Mungu anafanya hilo kwa Roho ya Neno lake (2Korintho3:6; Yohana 6::63). Anabadilisha. Anapanda mbegu zake, anamruhusu Roho wake aje juu ya hizo mbegu, na inaleta matokeo. Roho wake Mtakatifu anabadilisha zile mbegu za Neno ili ithibitishe ni aina gani.

Wewe ni mbegu ya aina gani? Hilo linaonyesha na kile kilicho ndani yako. Huwezi kulifanya hilo. Kile ulicho ndani kinaonekana nje. Huwezi kukizuia. Huwe ukaufanya ule mti chochote ila kile ulicho. Unaona, itaenda kuwa hivyo. Roho Mtakatifu anabadilisha hizo mbegu ndani ya huo. Haijalishi ni mbegu ya aina gani, itaibadilisha hiyo. Kama ni ovu, itazaa uovu. Kama ni Nafiki, itazaa mbegu ya kinafiki. Kama ni mbegu halisi ya Neno la Mungu, itaenda kuzaa wana na binti halisi wa Mungu.

Ni wangapi hapa ambao hawana mbegu ya Mungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu? Mngeweza tu kuinua mikono yenu na kusema, nikumbuke mimi, ndugu Branham. Kwamba nitampokea huyo Roho mtakatifu. Sasa ulichukuwe Neno moyoni mwako, na uliamini.
Unaweza ukajiangalia. Nenda ukajiangalie kwenye kioo na unaweza kuona uko mahali gani. Unaona. Unaweza kujua. [5]

Nilikuwa nazunguza na mtu siyo muda mrefu uliopita, alikuwa anajaribu kujadiliana nami na kusema, "Huoni aibu kusema kuwa Mungu aliumba mbingu na nchi katika muda wa siku tatu au katika siku sita?

Nikasema, "Hivyo ndivyo Biblia imesema

Akasema, vema, tunao ushahidi na tunaweza kuthibitisha kuwa dunia ina umri wa mamilioni ya miaka"

Nikasema. Hilo halihusiani kabisa na hilo. Katika mwanzo 1:1 imesema Hapo Mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Muda. Unaona? Ndivyo hivyo tu. Sasa, dunia ilikuwa ukiwa mtupu". Nami nikamwambia Ninaamini kila mbegu ilikuwa imelala hapo. kutokana na ustaarabu mwingine au kitu fulani, na mara tu maji yalipoondolewa na Nuru ikapiga hiyo, ikamea miti na kila kitu kinginecho.

Kadhalika na viumbe vya wanadamu; ni mfano. Wakati ukungu wote unapoondolewa, na ukweli ukafunuliwa kwa mbegu ya kweli iliyolala pale ambayo ina uhai, na Nuru ya injili ikaipiga hiyo kwa uthibitisho wa kweli wa Neno, itaishi; ina uhai ndani yake……. Nje ya hapo haiwezi kuishi, kwa maana haina uhai ndani yake. [6]

Mwangalie yule mwanamke pale kisimani (Yohana 4:1-30), ilikuwa ni nini? Ile nuru iliipiga ile mbegu, ambayo ilikuwa imelala pale ambayo ilinenwa na Mungu. Ndiyo Bwana ile mbegu ilikuwa duniani. Wakati Mungu alipoyaondoa maji na jua lilipiga ikakua; hiyo ni sawa. Unaona? Hicho ndicho tu ilichohitaji ni jua. Ilihitaji Nuru. Ndiyo Bwana.

Na sasa wakati Roho mtakatifu Ndani yake aliondolea mbali ndani yake maisha ya zamani na akamuonyesha yeye, kuwa nuru imeipiga; na akasema "Bwana, naona wewe ni Nabii".

Hiyo ndilo jambo hilo hilo leo, jambo hilohilo. Inapiga pale tu, ndiyo Bwana, alijua hilo kwa sababu Nuru imeipiga hiyo.

Wale wavuvi, watu wa misituni, wakulima, washika kodi; makahaba, walio ndani yake kile ambacho maandiko rahisi yalisema, Angeweza kufanya na mafarisayo wasingeweza kuona kwa sababu ya kanuni zao Amen. Wasingeweza kuona kwa sababu ya kanuni zao. Lakini yule kahaba, mkuliwa, na wengineo wote, walio na hilo. Wote waliokusudiwa kimbele, shaka zilipoviringika mbali, ile mbegu ilienda kukua, hiyo ni sawa. [7].

Sasa kama unataka ubatizo wa Roho mtakatifu, ni wa kwako, kama uko tayari kufungua moyo.

Sasa una mawazo ya kile unachopaswa kufanya. Una wazo la aina fulani. "Vema sasa, kama nitasimama hapa hivi" hapana hapana. Unaweza ukakaa chini. Haifanyi tofauti yoyote kama uko mahali gani. Lakini mahali ambapo ungefungwa mwenyewe, na halafu Roho Mtakatifu ataingia hapo.

Halafu, vema wakati mwingine inaanza kwa kukupaka mafuta wewe na sio utaongoza tu nayo kote. Unafika mahali unaogopa kidogo. Unaogopa unarudi nyuma. Jisalimishe tu, jisalimishe mwenyewe kwa Roho Mtakatifu.

Usiogope habari ya uzushi, kama ni shetani anatenda Je hujui sisi tutalijua hilo? Ndiyo Bwana, hatakuja hapo. Usiogope juu ya hilo. Hapana. Hatasumbua ndugu.

Jisalimishe tu wewe mwenyewe kwa Roho Mtakatifu. Unapoanza kusikia ile hali ya utukufu….. kama huyu mhuduma mdogo alisema alichofanya ule usiku, akiwa amesimama, kitu fulani cha joto (kidogo) kikaja karibu naye.

Kama tu angejua kujisalimisha tu wakati huo yeye mwenyewe. Hivyo tu sema tu "Bwana Yesu ninakuamini wewe". Nina kukubali wewe. Hapo sasa kitu fulani kitaanza kufanya kazi. Unaona? Maanisha hilo kutoka moyoni mwako, halafu sasa inafanyika oh. [8]

Hapa ipo siri: Ile siri ni maandiko-ambayo ni" ukweli fulani ambao ulifichika, lakini sasa unafunuliwa kiungu; lakini bado kunahali ya ki muujiza ambayo bado ina bakia,pamoja na kufunuliwa. Hapa ni moja ya siri hiyo kuu:

Ile siri ya ubatizo waRoho Mtakatifu bila msisimko,lakini ule utu wa Yesu Kristo unatenda ndani yako.kazi zile zile ambazo Yeye alizifanya. [9]

Unatafuta baraka za Mungu,unatafuta Neno lake unatafuta Roho Mtakatifu,unatafuta upendeleo wa Mungu.na hasa kama uko hivyo na unaweza hasa kwa moyo wako wote,kuusalimisha huo;sasa usiangalie msisimko.Angalia ukweli (Yohana 8:31-32).Ukweli ambao unatoka moyoni,kwa imani "Bwana niko tayari kufanya chochote ambacho Neno lako litaniamuru nifanya.Nijisalimisha mwenyewe, pamoja na vyote vilivyo ndani yangu [10]

Sasa, kama mtu ana huzuni kwa dhambi zake………nataka kulichukuwa kirahisi, ililizame ndani hasa.Kama mtu anasikitikia/kujutia dhambi zake na anatubu,akiwa anasikitika kwa dhambi zake,na anamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wakekutokana na dhambi zake, na anabatizwa kwa jina la Yesu Kristo, Mungu anawajibika katika wakati ule ule kumpa huyo mtu ubatizo wa Roho Mtakatifu.Kama siyo, Hawezi---hakushika Neno lake,Je hiyo ni kweli? Sasa, kwa nini mikutano yote ya kungoja tena? Kwanini ishara zote na mambo tunayotaka kuwa nayo? [11]

Yakupendeza sana.Mungu alimchukuwa Kristo,pale msalabani,akamchana vipande,Nafsi na Mwili.Akauchukuwa mwili juu kwenye mkono wake wa kuume na akamtuma tena Roho Mtakatifu,likiwa ni Agano na watu. Na unaamini kwa imani kama Ibrahimu alivyofanya; na akapewa muhuri ya kutahiriwa kwa uthibitisho wa imani yake (Warumi.4:9-12).Na unaamini na kumkubali Yesu kama Mwokozi wako, halafu Mungu anakupa ubatizo wa Roho Mtakatifu kama uthibitisho wa imani yako.

Unasema unaamini, na hujapokea Roho Mtakatifu, kuna kitu siyo sahihi na imani yako.Mungu anautahiri moyo dakika ile ile Amen.Semeni hilo enyi watu, hakika lazima kumefanyika jambo fulani; nimejisikia hivyo nilipokuwa nimekuja.Lipate hilo.wakati muaminio…..Liko hapa sasa. Wakati muaminio anapoamini kwa uthabiti juu ya Bwana Yesu Kristo, Mungu analazimika kumpa huyo Roho Mtakatifu; uthibitisho wa imani yake.Unasema, kuna nini ndugu Branham?" ni imani yako tu; kama kwa hakika umeamini.Mungu yuko pale kukupa wewe hilo.

Wakati Petro anazungumza haya maneno,Roho Mtakatifu aliwashukia wale walioamini lile Neno. Ni sawa hiyo? Matendo 10:49.vema, angalia Roho Mtakatifu na moto ulikuja kutoka mbinguni (Mathayo 3:7-12).ikateketeza uchafu wote,na kutahiri moyo,ikakata nyama yote iliyozidi, na kuwa kiumbe kipya (Wagalatia 6:14-16). [12]

Na hapa ndipo Mungu alipozungumza kutoka mbinguni, na Yohana mbatizaji alimuona Roho wa Mungu akija kama huwa, akishuka juu ya mtu ambaye amezaliwa katika hori la ng'ombe (Yohana 1:29-34). Unaona.Vile dunia inachokiita kikubwa. Mungu anakiita upumbavu. Na kile ambacho dunia inakiita upumbavu, Mungu anakiita kikuu.Hiyo ni sawa .Kwa hiyo usijali kuitwa mpumbavu.

Kwa sababu kumbuka,huwezi ukawa na akili ya Kristo na akili ya ulimwengu kwa wakati mmoja (Filipo 2:5-8) huwezi ukawa katika njia yako na njia ya Mungu wakati huo huo.Itabadi uondoke katika njia yako mwenyewe ili kumruhusu Mungu awe na njia yake.Hiyo ndiyo njia pekee kama utaenda kufanya chochote.Inabidi uondoke mbali kutoka kwenye mawazo yako, kufikiri kwako,usijaribu kuwaza amini tu.Ni vipi kama Maria alianza kuwaza juu ya kuzaliwa upya au hapana siyo kuzaliwa upya,lakini ni uzazi wa bikira (Matayo 1:18-25;Luka 1:26-38).

Nisikilizeni. Ni vipi kama angesema,sasa,ngoja kidogo.Sasa angalia.Sijui mtu yoyote kama hivyo.Nitaweza kuwa na mtoto? oh huwezi ukaniambia hivyo.Hakungojea chochote kamwe.Alimchukuwa Mungu kwenye Neno lake na akaanza kumshukuru Mungu kwa ajili ya mtoto.Kabla ya ishara yoyote kutolewa kwake,alichukuwa lile Neno la Malaika na akaenda akifurahi na kumsifu Mungu,alimuambia kila mtu kuwa ataenda kupata mtoto,bila kumjua mume [13]

Alisema " na iwe kwangu sawa na Neno la Bwana" hiyo iliuleta uhai.Tuko hapo vema, ulijua shetani alimuambia "watu wote wanakucheka wewe"

Yule msichana mdogo mwenye mashavu ya kupendeza,hakusikiliza hilo.Akaenda Yudea na alienda na kusema, "unajua,ninaenda kupata mtoto"kabla hajasikia chochote,kwasababu Neno lilikuwa limekaa pale.Hilo lilitosha.hakuhitaji kwenda kwenye mstari wa maombi mara ya pili.Hapana……Ndiyo,bwana,aliliamini hilo.hakuwa na ishara yoyote ya uhai;hakuwa na ishara yoyote ya kuwa na mimba hata kidogo;hakusikia chochote;kila kitu kilikuwa kama kilivyo kuwa, lakini alienda akimwambia kila mtu, ninaenda kupata mtoto" Kwa nini?Mungu alisema hivyo.Ni nini? Ule uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

Oh, kila mmoja anaweza kusema hivyo leo? Oh, kama watu kutoka miongoni mwao, sisi sote tungeweza kusema hivyo:na iwe kwangu sawa na Neno lako Bwana,ukimaanisha hivyo hasa.Mmoja au wawili au penginepo popote nje kule wataenda kulinasa hilo, waliochaguliwa kimbele ambao wanamaanisha hilo hasa,na ndugu, utaenda kuona cheche zikiruka wakati huo(Hiyo ni kweli) unapokuwa unacho hicho kukabiliana na kile kinachokuja, unywesheaji huo unapoanza kuanguka katika Neno.Ndiyo.bwana [14]

Mungu tupe akina Maria wengi mazingira ya hapa Phoenix,ambao wanaweza kumchukuwa Mungu katika Neno lake na kuanza kufurahi kabla chochote hakijatukia. Hicho ndicho unachohitaji. Hilo tu, kwa maana alifunikwa na Roho Mtakatifu.na wakati Roho Mtakatifu kwa ukweli anapomfunika mtu, wanamchukuwa Mungu kwenye Neno lake. hilo linamaliza, ni kile Roho Mtakatifu alichosema. [13]

Hatua za kusudi la milele alilokuwa nalo katika siri yake sasa imefunuliwa. Angalia, bado kuna hatua tatu za kwenye ukamilifu. Kama vile tu anavyoikomboa dunia; hivyo hivyo ndivyo alivyolikomboa kanisa lake.Anawakomboa watu katika ngazi tatu.Sasa angalia kwanza ni kuhesabiwa haki kwa imani,kama vile Luther alivyohubiri; pili, utakaso, Kama Wesley alivyohubiri; tatu, ubatizo wa Roho Mtakatifu.Hiyo ni sawa.Halafu sasa unakuja unyakuo!

Sasa,dunia, ameikomboaje dunia? Kitu cha kwanza, alichofanya, ilipotenda dhambi, aliifutilia mbali katika ubatizo wa maji. Hiyo ni sawa.Halafu akamwaga Damu yake juu yake, kutoka msalabani, na akaitakasa na kuiita kuwa ni yake na baada ya hapo anafanya nini? Kama alivyouchana chana ulimwengu utoke ndani yako,na kuufanya upya kitu chote na moto wa ubatizo wa Roho Mtakatifu.Yeye ataifanya upya dunia na itachomwa juu ya moto, na kusafisha kila kamdudu.(germ), kwa mamilioni ya maili kwenda juu.Kila kitu kitasafishwa. Na halafu sasa kutakuwa na mbingu mpya na nchi mpya, kama tu wewe ulivyo kiumbe kipya ndani ya Yesu Kristo wakati Roho Mtakatifu anapokujaza.unaona.pale ulipo. Kitu chochote kiko wazi kama iwezekanavyo kuwa.kila kitu kiko katika utatu.

Kuzaliwa kiasili kuna vitu vitatu,cha kwanza kutokea ni nini kwa mwanamke anayeenda kuzaa? kinaanza nini? Maji,kinachofuata ni damu .ni hatua gani nyingine uhai, maji, damu na roho. [15]

1Wakoritho 12:3. kwa hiyo nawaarifu, yakuwa hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema Yesu amelaaniwa……..hakuna awezaye kusema ……Yesu Kristo ni Bwana,ila ni kwa Roho.

Huwezi ukajua lolote juu ya hilo.mpaka lifunuliwe na Roho Mtakatifu.Unasema "ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu" umepokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini? (Matendo 19:1-7) kama bado, huwezi kumwita Yeye kuwa ni Bwana, kwa sababu siyo Bwana, ni kiumbe cha historia wewe kwa imani umekubali.Lakini anapokuja ndani yako kwa njia la Roho Mtakatifu.Yeye ni Bwana.Hakuna mtu anayemwita Yesu Bwana, mpaka tu kwa Roho Mtakatifu, mpaka amezaliwa kwa Roho wa Mungu, na Roho Mtakatifu yuko ndani yako…..na sasa kama uko hivyo,umezaliwa katika

ufalme wa Mungu, na u sehemu ya kanisa. Ninyi ni wale walioitwa watoke. [16]

Angalia tunaona watu leo, kuna watu wengine hawawezi kuliamini hata watu waliojazwa na Roho. Nitaenda kuwapa moja ambalo litawapalia, Ubatizo wa Roho Mtakatifu haumaanishi kwamba wewe utaingia, hata kidogo, siyo hilo hapo, halihusiani na nafsi yako. Huo ni Ubatizo unaona. Hapa unaona ndani kule nafsi, hapa, inabidi iwe imetoka kwa Mungu. Lakini sasa huku nje unazo hisia tano, na tano za mawasiliano ya nyumba yako ya dunia. Kule ndani, unayo roho, na hapo kuna hisi tano dhamiri, na upendo, na kadhalika, hisi tano kuwasiliana na roho. Kumbuka katika roho unaweza ukabatizwa na Roho halisi wa Mungu na bado upotee. Ni ile nafsi ndiyo iishiyo, ambayo ilikusudiwa na Mungu.

Je Yesu hakusema wengi watakuja kwangu siku ile na kusema. Bwana, je sikutoa pepo, na kufanya kazi kuu, kutoa unabii, na vipawa vikuu vya Mungu? Akasema. Ondokeni kwangu ninyi mtendao uovu. Kamwe sikuwajua ninyi. (Matayo 7:21-270. “Wengi watakuja katika siku ile”.

Je kayafa hakutabiri? (Yohana 18:12-14). Alikuwa shetani,. Tunaona pale…… Na wale makuhani, wale watu wakuu, walipaswa kuwa viongozi wakuu katika siku zile, wakiwa wanyenyekevu na kila kitu, lakini walishindwa kuliona Neno la Mungu lenyewe likidhihirishwa mioyoni mwao. [17]

Kadhalika na balaam (Hesabu 13:5-30; 24:1-25). Hilo sio lolote…. Ninao ubatizo, wa Roho Mtakatifu. Hilo bado halina uhusiano wowote na hilo. Hiyo ni vipawa tu vya muda kwa ajili yako.

Kipawa halisi ni ndani hapa nafsi yako. Unaona. Ambayo imezaliwa na Mungu, na hiyo inatawala kila kitu kwenye Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu. Na pale ndiyo unakulia juu, unaona, halafu sasa ni mwana au binti wa Mungu. Ni mtoto wa Mungu. Vema mimi ni mpentekoste ndiko niliko. Kama huwezi ukalingana na hilo Neno kuna kitu sio sahihi. Unaona? Sasa, unaona baba yako hasa siyo Mungu unaona? Kwa sababu, Nafsi yako ndiyo mwanzo halisi/kabla hakujawa na roho, ilikuwa ni nafsi yako. Hiyo nafsi haikutoka kwa Mungu. Kwa hiyo haikuwa chembe ya Mungu, kwa kuanzia. Umedanganyika. Uko miongoni mwa magugu na unazaa rekodi ya dunia ya magugu yakuwayo. Unatenda kama dunia /ukipenda dunia ni kwa sababu upendo na Mungu hauko ndani yako.

Na sasa kutakuwepo wapakwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho, siyo Yesu wa uongo. Hawatasitahimili hilo. Lakini wapakwa mafuta wa “uongo” (Matayo 24:24). Wamepakwa mafuta, ndiyo Bwana lakini ni wapinga Kristo. Wamepakwa mafuta na Roho, kufanya ishara na maajabu ambayo Kristo alifanya. Lakini hawatataka kulingana na Neno lake. [18]

Mungu aliahidi Roho Mtakatifu kwa kila muaminio. Anataka akupe huyo, kuliko unavyotaka kumpokea Yeye. Sasa, usimwambie namna unayotaka kumpokea; Mwambie unamtaka. Haijalishi anakujaje, unamhitaji. Unataka kitu fulani moyoni mwako uweke nanga na nafsi yako, mpaka mashaka yote, hofu zote zimeondolewa na kengele za furaha ya mbingu zitapiga katika Nafsi yako. Mungu atashuhulikia yaliyo baki, wewe mweleze tu Yeye akupe ubatizo wa Roho Mtakatifu. [19]

Pengine mmoja kule chumba cha juu (kule nyuma wakati wa Pentekoste, (Luka 24:48-53). Alisema “kwa nini, naamini tumengoja vyakutosha muda mrefu. Hebu tukubali kwa Imani”. Hilo lilikuwa fundisho zuri la kibaptist, lakini halikutenda kazi kwa hawa wandugu. Kwa hiyo, unajua jambo la kwanza, inabidi iwe ni ukweli wa dhahiri, na walisubiri huduma yao kwa lile Neno kuthibitishwa. Na unapokuja kumtafuta Roho Mtakatifu, unafanya hivyo hivyo.

Ndiyo, unaweza kulikubali kwa Imani; unaweza umkubali Kristo kwa Imani; hiyo ni sawa kabisa. Na unamkubali Roho Mtakatifu kwa Imani, lakini sasa muache Roho Mtakatifu aje na akupe ishara ya kule kutahiriwa ushuhuda kwamba ameikubali Imani yako. Unaona.

Unaona. Ibrahimu alimwamini Mungu na kwake ikahesabiwa kuwa haki. Lakini Mungu alimpa yeye Ishara ya kutahiriwa kama uthibitisho kuwa ameikubali Imani yake. Kwa hiyo tunapaswa kufanya hivyo hivyo. Tunapaswa kumngojea Roho Mtakatifu mpaka awe amefanyakitu fulani, siyo lazima kwamba tumenena kwa lugha, siyo kwa sababu tumecheza, au tunamsisimko, tumepiga kelele: mpaka tumebadilishwa, mpaka kitu fulani hasa kiwe kimetokea. Sijali kinakuja kwa namna gani, ili mradi kinatokea; hilo ndilo jambo muhimu. [6]

Ndugu Braniham aliulizwa swali hili: wakati ule hasa wa kupokea Roho Mtakatifu au ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuna kuwa na tofauti? Je mtu ana nena kwa lugha? Kama siyo kila siku, ni kwa udhihirisho gani inajulikana?

Vema ungewaza vipi mama anazaa mtoto na bila kulijua hilo? Inabidi awe amepoteza fahamu zake ili asilijue hilo. Kadhalika huwezi kupokea Roho Mtakatifu bila kujua hilo. Kuna kitu kinafanyika ndani yako. Unaona? Kuna kitu fulani ambacho kinakubadilisha wewe. Mfumo wako wote. Mfumo wako wote wa kiroho unafanywa mpya tena, na unakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo, kama Biblia inavyo liweka hilo. Uumbaji mpya ndani ya Kristo (2Korintho 5:17). Unalijua hilo.

Sasa unasema, “Ndugu Branham, sasa huamini kwamba mtu lazima anene kwa lugha ili kupokea Roho Mtakatifu”. Siyo kuthibitisha kwamba ana Roho Mtakatifu.

Ningependa kila mshirika hapa kanisani kwangu anene kwa lugha. Nimgependa wao wafanye hivyo, na ninaamini kama utamuomba Mungu, Mungu atakupa hilo. Lakini ngoja nikuambie: ninawajua watu wengi ambao wananena kwa lugha na hawana Roho Mtakatifu. Na hakuna mhuduma ambaye ni mkweli kwa nafsi yake na kusanyiko lake ila ataliambia kusanyiko lake hivyo hivyo.shetani anaweza kuigiza hilo.

Paulo alisema,hata ningenena kwa lugha za wanadamu na za malaika,hata ningetoa mwili wangu niungue moto kama sadaka,hata kama

ningeelewa na siri zote za Neno.hata ningetoa mali yangu yote niwape maskini,na mambo haya yote,na kama sina upendo bado mimi si kitu,ningekuwa hata na imani ya kuhamisha milima na kadhalika,bado si kitu mimi (1 Kor 13:1-13) halafu akasema ile iliyo kwa sehemu itabadilika wakati ile iliyo kamilifu itakapokuja" au ile iliyo kamili itakapojulikana. [20]

Kwa hiyo kama Mungu amekuponya usiku wa leo, unaweza ukawa mgonjwa tena kabla ya kufa. Unaweza ukawa mgonjwa tena mwaka mmoja kutoka sasa, au miaka miwili kutoka sasa, au siku moja kutoka sasa, sijui, lakini kuna jambo moja la uhakika, utakuja kuondoka hapa duniani moja ya siku hizi, kwa sababu hii ni kiraka tu.

Lakini kama ile nafsi itakutana na Roho Mtakatifu na ikazaliwa mara ya pili,unao uzima wa milele. Haijalishi kutatokea nini hapa, kamwe hutakufa.Yesu aliyenituma anao (hiyo ni usemi wa sasa) uzima wa milele, hataingia hukumuni; lakini (usemi uliopita) amepita kutoka mautini kuingia uzimani" hiyo ingetufanya sote kuwa wamethodist na kuanza kupiga kelele. si ndiyo hivyo? Hiyo ni kweli.kufikiria hilo, kwamba Mungu amefanya hilo. Sasa hayo siyo yangu;hilo ni lake Yohana Mtakatifu 5:24. [21]

Sasa,Roho Mtakatifu yuko hapa duniani,akiangalia watu wale ambao Mungu aliwakusudia uzima wa milele katika wakati huu.Na mara tu wanapoupata, inafanya kama ilivyokuwa ndani ya Yesu Kristo.Yule mtoto Mkuu wa kimiujiza Mwana wa Mungu aliyetukomboa sisi sote.Inakuja chini na kuchukuwa mahali pake pa kupumzikia ndani ya maisha ya binadamu. Sasa angalia, imeleta ile nguvu ya kuhuisha (Warumi 8:11). Sasa ile nguvu ya kuhuisha ambayo imekuja juu ya Yesu na kumhuisha Yeye ili kudhihirisha kila ahadi ya Neno la siku ya leo. kadhalika Roho Mtakatifu ambaye amekuja juu yetu katika siku hii. Kama siyo Roho Mtakatifu wa dhihaka,wewe siyo shetani kudhihaki Roho Mtakatifu.Lakini ni halisi,Roho Mtakatifu wa Kweli.Atadhihirisha ahadi za saa hii.

Alipomwangukia Luther,alidhihirisha lile Neno la ahadi la saa ile.alipomshukia Wesley, alidhihirisha Neno la ahadi la saa ile.anaposhuka katika siku ya leo anadhihirisha ahadi za saa hii.aliposhuka juu ya Musa, alidhihirisha ahadi ya saa. Aliposhuka juu ya Noah, alidhihirisha ahadi ya saa ile. Aliposhuka juu ya Yesu, alidhihirisha ahadi ya saa ile. [22]

Maombi ya nabii;sio tu wabatizwe na maji, ambayo ni ishara tu ya nje kwamba kitu fulani ndani kimetokea.Biblia ilisema, "kuna imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja"na ubatizo huo ni wa kiroho (Waefeso 4:4-6) mwili ukiwa umeoshwa, ni tu kielelezo au kutoa ishara.kwamba kitu fulani kimetokea ndani (Matendo 22:14-16).Lakini ni ile nafsi ambayo inapaswa ibatizwe na Roho Mtakatifu, ambayo ni kuja kwa umilele katika mwanadamu wa asili na kumbadilisha kabisa,kumfanya awe mwaminio.Ninaomba kwamba watapokea Roho Mtakatifu.Nawaweka mikononi mwako sasa, kama zawadi kwa ujumbe, na kwa neema ya Kristo.katika jina lake
ninaomba.Amen.[23]

Nukuu za kiingereza.


[1] Wakati wa kanisa la Smirna NSK)uk 154
[2] Ile ishara(63-1128) Aya 153
[3] Kitabu cha nyakati saba uk.144
[4] kule kunyakuliwa Aya 93
[5]Nguvu ya Mungu ya kubadilisha Aya 212-213
[6]Muhuri wa nne kitabu cha mihuri uk.289-292
[7]Muhuri wa tatu kitabu cha mihuri uk.260-261
[8]Mungu akijifunua katika urahisi(63-0412E) ,Aya 361-365
[9] Je huu ndio wakati? Uk 30-31
[10] Muungano usioonekana uk.56
[11] Uzima wa milele na namna ya kuupokea Aya82
[12]Israeli na kanisa sehemu ya 3.Aya 40-42
[13]Mashahidi (54-0303). Aya E-27-28
[14]Lile Neno lililonenwa ndio mbegu ya asili uk.28-30
[15]Huyu Melekizedeki ni nani Aya113-116
[16]Vitambulisho vitano dhahiri vya kanisa la kweli Aya 164-165
[17] Matukio ya leo yakiwekwa wazi na unabii Aya 100-102
[18]Mambo yatakayokuwa Aya 111-114
[19] Mungu akilikamilisha kanisa lake Aya E-27-E-28
[20]Maswali na majibu swali no.289 COD uk 1017
[21]Ukombozi ni kwa nguvu Aya 9-10
[22]Muhuri ya pasaka Aya 89-87
[23] Sauti ya ile ishara Aya 192



*jiwe la kiroho la kujengea na 165 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*


*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*


*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*